



## ***Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo***

### **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21- 30 NOVEMBA, 2022 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01- 10 DISEMBA, 2022.**

#### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21- 30 NOVEMBA, 2022.**

Katika dekadhi hii migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuwa imedhoofika wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini (Azore na Siberia) ili endelea kuimarika kidogo. Hali hii iliendelea kuleta mchango katika kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) kuelekea nchini kwetu hususani katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na Magharibi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilionekana katika eneo la Magharibi mwa bahari ya Hindi wakati katika eneo la Mashariki ya bahari ya Hindi joto la bahari lilikuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani. Hali hii iliendelea kuleta mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya mwambao wa pwani ya nchi yetu hususani katika nusu ya pili ya dekadhi. Joto la bahari katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilionekana kuwa la juu kidogo ya wastani na hivyo kutokuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu.

#### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21- 30 NOVEMBA, 2022.**

Kwa ujumla, viashiria vya hali ya hewa hapo juu vilipelekea baadhi ya maeneo ya nchi kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi hasa katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, Magharibi mwa nchi pamoja na pwani ya Kaskazini. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi hadi mvua za wastani viliripotiwa katika maeneo ya nyanda za juu kusini-magharibi, Kusini, maeneo ya kati mwa nchi pamoja

na pwani ya Kusini.

## **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 DISEMBA, 2022.**

### **2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 DISEMBA, 2022.**

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) katika kipindi hiki inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini (Azore na Siberia) inatarajiwa kuwa imeimarika kidogo. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) kuelekea nchini kwetu hususani katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na Magharibi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la Magharibi ya bahari ya Hindi wakati katika eneo la Mashariki ya bahari ya Hindi joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani. Hali hii inatarajiwa kutokua na mchango mkubwa katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya mwambao wa pwani ya nchi yetu. Joto la bahari katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani na hivyo kutokuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu. Hata hivyo, kuimarika kwa wimbi anga (MJO) katika kipindi hiki kunatarajiwa kuwa na mchango katika kuimarisha utengenezaji wa mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

### **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE (01 - 10 DISEMBA, 2022).**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):**

Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vichache vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa hususani katika nusu ya pili ya dekad.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu na yenye vipindi vichache vya mvua nyepesi.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususani katika nusu ya pili ya dekad.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na;

## MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA